



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE



Unapojibu tafadhali taja:-

Kumb. Na. UA.12/290/01/22

19/02/2025

## TANGAZO LA KAZI YA MUDA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe anawatangazia nafasi 4 za kazi ya Muda ya kufyatua Tofali za Saruji(cement bricks) na anakaribisha maombi kwa watanzania waishio Wilaya ya Njombe wenye sifa na uwezo kwa ajili ya kujaza nafasi ya kazi kama ilivyo orodheshwa katika tangazo hili. Aidha mnajulishwa kuwa mwisho wa maombi haya ni tarehe 21.02.2025 hadi 28.02.2025

### 1. KAZI YA KUFYATUA TOFALI - NAFASI 4

#### (a) Sifa za mwombaji.

Mwombaji mwenye elimu kuanzia Darasa la saba na kuendelea(ajue kusoma na kuandika), mwenye Afya njema, awe na nguvu za kutenda kazi,awe muadilifu na mwenye kujituma na sifa njema kwa jamii.

#### (b) Eneo la kazi

Mashine ya Uzalishaji Tofali imesimikwa katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Njombe zilizopo Katika Kijiji cha Kidegembye Kata ya Kidegembye. Kazi hii itakuwa ya miezi mitatu na Muda wa kazi ni kuanzia saa 08:00 hadi 12:00 jioni kulingana na uhitaji wa kazi.

#### Kazi na majukumu

- (i) Kuendesha Mtambo wa kufyatulia tofali.
- (ii) Kufyatua Tofali na kuzipanga.
- (iii) Kumwagilia tofali na bidhaa nyingine zilizozalishwa.
- (iv) Kutunza kumbukumbu za malighafi na bidhaa zilizozalishwa.
- (v) Kutunza mali na vifaa vya Mradi

Barabara ya Kibena – Lupembe (Kata ya Kidegembye Kijiji cha Kidegembye), SLP 547 Njombe, Simu: +255 26 2782111 (Mkurugenzi), +255 26 2782027 (Maulizo), Nukushi +255 26 2782857 Barua pepe: info@njombedc.go.tz; Tovuti: www.njombedc.go.tz

(vi) Kuhakikisha mazingira ya kazi yanakuwa safi na salama muda wote.

## MALIPO

- (i) Malipo yatalipwa kwa kizio cha uzalishaji yaani Tsh.120 kwa kila tofali litakalozalishwa kwa timu nzima ya uzalishaji.

## 2. MAELEKEZO

- (i) Waombaji wote wawe raia wa Tanzania wasiozidi umri zaidi ya miaka 45 na wasiopungua umri wa miaka 18.
- (ii) Mwombaji aambatanishe barua ya Utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa eneo analoishi .
- (iii) Waombaji wote waombe kwa kufuata masharti ya TANGAZO LA KAZI YA MUDA,
- (iv) Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili.
- (v) Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 28.02.2025 saa 9:30 alasiri, baada ya tarehe hiyo kupita maombi hayatapokelewa na watakao chaguliwa watajulishwa
- (vi) Barua zote ziletwe kwa mkono Masijala ya wazi iliyopo Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Njombe iliyopo Kijiji cha Kidegembye kupitia anwani iliyobainishwa hapa chini.

MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE,  
S.L.P 547,  
**NJOMBE.**

Tangazo hili limetolewa na:-

  
Christopher A. Sanga  
MKURUGENZI MTENDAJI  
**HALMASHAURI YA WILAYA NJOMBE**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE  
S.L.P. 547  
NJOMBE**